

TANGAZO KWA UMMA

Mwenyekiti Mpya wa Bodi ya Wadhamini ya Women Fund Tanzania Trust



Prof. Penina Mlama

Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake Tanzania (WFT - Trust) inapenda kuutaarifu umma kwamba kupitia kikao chake kilichofanyika tarehe 11 August 2023, imemchagua Profesa Penina Mlama kuwa Mwenyekiti mpya wa Bodi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Prof. Penina Mlama anachukua nafasi ya Prof. Ruth Meena ambaye aliongoza Bodi hiyo akiwa Mwenyekiti wa kwanza.

Prof. Penina Mlama, ni mwanataaluma, mwandishi, msimamizi hodari na nguli wa ujenzi wa maudhui ya kimapinduzi katika masuala ya jinsia, sanaa ya maonyesho, maendeleo na elimu. Pamoja na hayo, Prof. Penina pia ni mbobevu kwenye masuala ya uongozi na amewahi kutumikia kwenye Bodi kadhaa ikiwemo Taasisi ya Mwl. Nyerere, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) na Chuo Kikuu cha Mtakatifu John.

Kabla ya kuchaguliwa kwake, Prof. Penina Mlama alikuwa mjumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake Tanzania na kuifahamu vyema falsafa ya kifeminia ya utendaji wa mfuko huu.

Uongozi wake kama mwenyekiti mpya wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake Tanzania (WFT-T) ulianza rasmi mnamo tarehe 13 Disemba 2023 baada ya kumalizika kwa kipindi cha uongozi wa mpito.

Bodi inachukua fursa hii kutoa shukrani zake za dhati kwa Prof. Penina Mlama kwa kukubali jukumu kubwa la kuongoza na kusimamia Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake Tanzania (WFT - Trust).

Vile vile Bodi inamshukuru Prof. Ruth Meena ambaye amekuwa na mchango mkubwa sana katika ujenzi wa Mfuko wa Ufadhili wa Wanawake na amesimamia mabadiliko chanya ya kiutendaji na kimfumo katika kipindi cha uongozi wake mahiri.

Tunakupongeza na kukutakia kila la heri Profesa Penina Mlama. Karibu sana

**Imetolewa na :
Sekretariat ya WFT-T**